

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/2203158

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua pepe : ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,

3, Barabara ya Rashid Kawawa,

S.L.P. 5429,

12880, DAR ES SALAAM.

Tanzania

03 Januari, 2021

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

RC KUNENGE APOKEA MAGARI 20 NA KONTENA 65 ZA KUHIFADHI TAKA.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Aboubakar Kunenge leo March 03 amepokea Magari 20 na Kontena 65 za kuhifadhi taka zenye thamani ya Shilingi bilioni 4.1 ambapo amewahimiza wakazi wa Dar es salaam kuhakikisha wanazingatia suala la usafi wa mazingira.

Akipokea Magari hayo kwenye Bandari ya Dar es salaam, RC Kunenge ameyagawa kwa Halmashauri zote za Dar es salaam ambapo Halmashauri ya Jiji imepatiwa Magari 5, Manispaa ya Temeke Magari 8, Kinondoni Magari 5, Ubungo Gari 1 na Kigamboni Gari 1.

RC Kunenge amewaelekeza Wakurugenzi wa Manispaa zote kuhakikisha suala la usafi linapewa kipaombe huku akitaka magari hayo kutunzwa ili yadumu Muda mrefu na kutatua kero ya usafi.

Aidha RC Kunenge ametoa wito kwa wananchi kuepuka tabia ya kutupa taka kwenye mitaro na mito kwani kwa kufanya hivyo wanasababisha mitaro kuziba huku akisema watakaohusika kuchafua mazingira Sheria itafuata mkondo.

Kwa upande wake Mratibu wa Miradi ya Bank ya Dunia chini ya TARURA na DMDP Humphrey Kanyenye amesema lengo la miradi wanayosimamia ni kuhakikisha

wanaboresha mazingira ya Dar es salaam ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira kuwa Safi.Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM